JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILYA YA HANANG'

SHULE YA SEKONDARI HANANG

S. L. P 218

KATESH – MANYARA

02/12/2022

Kumb.Na. HSS/ MKS/K1. 2023

MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI .....

S. L. P .....

.....

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI HANANG WILAYA YA HANANG' MKOA WA MANYARA, KIDATO CHA I, 2023**

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari HANANG kidato cha kwanza mwaka **2023. Hongera sana**. Aidha kwa niaba ya Bodi ya shule, walimu na wafanyakazi wa Shule ya Sekondari Hanang ninakukaribisha **"karibu sana shule ya Sekondari HANANG".**

1.1 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari **Hanang** ipo katika kijiji cha Nangwa , kata ya Nangwa, Tarafa ya Katesh, Wilaya ya Hanang' katika mkoa wa Manyara. Shule iko pembezoni mwa barabara ARUSHA-SINGIDA. shule ipo umbali wa kilometa 8 kutoka makao makuu ya wilaya. Usafiri wa kufika shuleni unapatikana kuanzia asubuhi hadi saa mbili na nauli ni shilingi 1000/- kutoka stendi ya mabasi kateshi hadi shuleni.

1:2 TAREHE YA KURIPOTI

Mhula wa masomo kwa mwaka 2023 unaanza **tarehe** 09/01/2023. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 09/01/2023 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/01/2023.

Ufikapo shuleni fika ofisi ya mkuu wa shule kwa ajili ya usajili. Hairuhusiwi kuingia darasani kabla ya kusajiliwa.

1:3 AINA YA SHULE

Shule hii ni ya kutwa kwa wanafunzi wote wavulana na wasichana kidato cha kwanza hadi cha nne.

Mawasiliano hapa shuleni ni kwa lugha ya kiingereza.

1:4 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1 Sare za shule

Sare za shule na rangi zake

WAVULANA

1. Suruali mbili za kijani (jani la mgomba)
2. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
3. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kufunga na kamba, visiwe buti
4. Jozi mbili ya soksi ya khaki
5. Tai ndefu yenye rangi sawa na suruali
6. Sweta ya rangi ya kijani (jani la mgomba) yenye shingo ya "V" isiyopasuliwa mbele
7. Tshirt ya shule, utaratibu utatolewa mara baada ya wanafunzi kuripoti
8. Viatu vya michezo na nguo za michezo yaani (Tshirt kijani na bukta ya njano)
9. Saa ya mkononi
10. Pullneck nyeupe (kaba shingo)kwa ajili ya kuzuia baridi

***** suruali inayobana, mnyonyo na mlegezo haviruhusiwi *****

WASICHANA

1. Blauzi mbili (2) nyeupe mikono mifupi
2. Sketi mbili (2) marinda madogo ya kawaida kumi na mbili sita mbele sita nyuma ya **kufunika soksi**)
3. Kwa waislamu washone sketi (jani la mgomba) ndefu kabisa inayofunika soksi
4. Jozi mbili za viatu nyeusi visivyo na visigino virefu vya kufunga na kamba
5. Jozi mbili za soksi nyeupe ndefu
6. Sweta ya rangi ya kijani (jani la mgomba)yenye shingo ya " V" isiyopasuliwa mbele
7. Tshirt ya shule, utaratibu utatolewa mara baada ya wanafunzi kuripoti

8. viatu vya michezo na nguo za michezo yaani (Tshirt ya blue na bukta nyekundu)
9. Tai ndefu yenye rangi sawa na sketi
10. Saa ya mkononi
11. Pullneck nyeupe (kaba shingo) kwaajili ya kuzuia baridi
12. Kwa waislamu jalabibi/ushungi uwe wa rangi nyeupe, jalabibi/ushungi iwe ndefu kuvuka kiunoni na sketi zao ziwe ndefu hadi vifundo vya mguu. Ushungi usiwe na urembo, kitambaa cha jalabibi/ ushungi visiwe vyenye kuangaza (transparent). Blauzi nyeupe na yenye mikono mirefu.

Unatakiwa kuwa na jozi mbili za viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi na vyenye kufunga na Kamba (gidamu) visivyo na visigino virefu. Viatu maarufu kwa jina la bajaji , raba na aina nyingine kama hiyo hiviruhusiwi shuleni.

NB: Uvaaji wa sare za shule ni muhimu na ni lazima uwe na sare ya shule yenye heshima na itakaguliwa ukifika shuleni kama tulivyokuagiza katika fomu hii.

1.2 Vitendea kazi darasani

I. Madaftari makubwa 10 (counter book quire 3) yakuandikia notes
II. Madaftari madogo yakutosha yenye kurasa 48 au 96 ya kufanyia mazoezi
III. Jalada (spring file) la kutunzia mitihani unayoifanya
IV. Kalamu za kutosha, penseli, rula, kifutio cha penseli na mkebe wa vifaa vya mahesabu (mathematical set), kamusi ya kiingereza (dictionary)
V. Rim moja kwa ajili ya majaribio mbali mbali ili kuepuka kuchana karatas kwenye madaftari.
VI. Ufagio, ndoo ndogo, na jembe lenye mpini imara na kwanja kwaa jili ya usafi wa darasa na mazingira ya shule

1.3 Chakula cha wanafunzi na mahitaji yake

Ni jukumu la mzazi kuleta chakula cha mtoto wako awapo shuleni na jamii kwa ujumla

Mahitaji ya wanafunzi wa kutwa

- Mahindi debe tatu (3) kwa mwaka
- Maharage debe moja (1) kwa mwaka
- Mchango wa mpishi Tsh 10,000/= kwa mwaka
- Mchango wa Taaluma Tsh. 10,000/= kwa mwaka
- Mchango wa chakula Tsh 40,000/= kwa mwaka (fedha hizi zitatumika kununua kuni, mafuta ya kupikia, sukari, chumvi, nyanya, vitunguu n.k)
- Vyombo vya chakula kama vile kikombe cha uji, sahani na kijiko (vyombo hivyo viwe vya udongo ama vya bati

(aluminium)

1.4 MCHANGO WA TAALUMA

Mchango uboreshaji taaluma 5000/= kwa muhula (fedha zitatumika kulipa walimu wa fizikia na kilimo)

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1.5 Mambo yakuzingatia

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu. Kama mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa vizuri mara baada ya kuripoti shuleni:

I. Heshima kwa Viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

II. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

III. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio baada ya vipindi vya darasani (preparatrion)

IV. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

V. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

VI. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

VII. Kuvaa sare ya shule kikamilifu wakati wote unapotakiwa;

VIII. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

IX. Kutunza mali za Umma na mali binafsi.

X. Ni lazima mwanafunzi ahudhurie shule siku zote 195 kwa mwaka na kwa masomo yote kwa siku. **UTORO** wa shule/ vipindi ni **MWIKO**. Mzazi kama kuna shida tafadhali toa taarifa mara moja.

1.6 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE

I. WIZI

II. UASHERATI NA USHOGA

III. UBAKAJI

IV. ULEVI NA MATUMIZI YA MADAWA YA KULEVYA KAMA VILE UVUTAJI WA BANGI, COCAINE, MIRUNGI, KUBERI NA KADHALIKA.

V. KUPIGANA AU KUPIGA

VI. KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI YA UMMA

VII. KUDHARAU BENDERA YA TAIFA

VIII. KUWA MJAMZITO, KUPATA MIMBA AU KUSABABISHA MIMBA

IX. KUTOA MIMBA

X. KUOA AU KUOLEWA

XI. KUGOMA, KUCHOCHEA NA KUONGOZA AU KUSHIRIKI KUVURUGA AMANI NA USALAMA WA SHULE AU WATU

XII. KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI

XIII. KUWA NA SIMU YA MKONONI/LAINI YA SIMU

2.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

2.1 **Fomu ya daktari: Medical Examination Form** ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. Fomu imeambatanishwa

2.**2 Fomu ya maelezo binafsi na mkataba**: Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai imeambatanishwa na unatakiwa kuijaza na kuirejesha kwa Mkuu wa Shule. Sehemu ya pili ya fomu hii itajazwa na mzazi ihusuyo kukiri kukubaliana na sheria. Kanuni na maelekezo mangine yatakayotolewa shuleni.

HITIMISHO: Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA

……

ADV. NICOMEDI Q. KWAHHISON

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MAAGIZO YAKE

Fomu hii irudishwe shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi ikiwa imejazwa kikamilifu

1. MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina kamili, ……. Raia wa ……

Madhehebu ……

Tarehe ya kuzaliwa …… umri miaka …… mahali ulipozaliwa ……

Mahali unapoishi; kitongoji …… kijiji …… kata……

Tarafa …… wilaya …… mkoa ……

Anuani ya nyumbani; S. L. P ……

Namba ya simu ya mkononi ya mzazi/mlezi; ……

Mimi …… nimiesoma kwa makini maelekezo/ maagizo ya kujiunga na shule hii, pia sheria za shule kwa makini. Kwa heshima na kwa unyenyekevu mkubwa ninaikubali/ ninaikataa nafasi hii pamoja na masharti na sheria za shule kwasababu ……

……

2. MKATABA MAALUMU KWA MWANAFUNZI

Mimi…….. nimehiari kwa akili yangu timamu, kutoshiriki au kushawishi wanafunzi wenzangu na jamii kwa ujumla katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi **kutokuwa mtoro kabisa** wa shule au vipindi. Nikijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za shule.

Tarehe …… saini ……..

3. TAARIFA YA MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI

Uthibitisho wa kushirikiana na shule katika kumlea mtoto wangu

i). Jina kamili la Mzazi/Mlezi …….

Uhusiano …….

Anuani ya nyumbani: S. L. P ……

Umri …… kazi …… mahali pa kazi ……..

Kitongoji ……. Mtaa / Kijiji ……. Kata ……

Wilaya …… Mkoa …… uraia ……..

Namba ya simu ya mzazi/ mlezi …….

ii). Mimi …….. Mzazi/ Mlezi wa …… ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako nimesoma maelekezo/ Maagizo na sheria za shule kikamilifu. Ninakubali/ ninakataa nafasi hiyo ninaahidi /siahidi kutimiza mahitaji ya mtoto wangu na maagizo ya kujiunga na shule kwa muda wote uliopangwa kwa kufuata sheria na kanuni zilizopo. Nitahakikisha mtoto wangu anahudhuria **shuleni bila kukosa.** Aidha naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, ya wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa toa sababu

…….

……

……

Tarehe …… Saini ……

(Isainiwe na mzazi /Mlezi na si vinginevyo)

Kiambatisho namba mbili

CERTIFICATE OF
MEDICAL EXAMINATION

HANANG SECONDARY SCHOOL,

P.O BOX 218

KATESH – MANYARA

Date …….

Ref No. HSS/HCU/HD/2023

The Medical Officer,

Government Hospital/DDH …….

P.O Box …….

Dear Doctor

RE: SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

NAME OF PUPIL …… FORM I YEAR 2023

We shall be grateful if you will kindly examine the above named pupil and give us a report to undertake in our school well. Please remark and indicate against the item mentioned below:

I. X- Ray ……

II. Urine ……..

III. Stool examination ……..

IV. Physical fitness ... Eyes, limbs, Chest, Ears, Spleen, Abdomen, Speech ……

V. V. D ……

VI. Tuberculosis (T. B) ……

VII. Pregnancy test ……

A. **PRELIMINARY INFORMATION FROM THE PUPIL BEFORE THE DOCTOR**

Historical Background

S/N	DISEASE	YES/NO	S/N	DISEASE	YES/NO
1	Tuberculosis		10	Epilepsy	
2	Asthma		11	ENT Trouble	
3	Pneumonia		12	Skin disorder disease	
4	Heart trouble		13	Anemia	
5	Recurrent indigestion		14	Operations	
6	Jaundice		15	Serious accidents	
7	Dysentery		16	Chronic Malaria	
8	Kidney & urine trouble		17	Stomach trouble	
9	Nervous break down		18	Eye disorder	

OFFICIAL MEDICAL EXAMINATION REPORT

Weight…… Heart Beat …….. vision ……..E.CT ……..

Doctor's Name …… Designation …….. Date ……..

Signature and Official Stamp, ……